FORM TWO HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI 10 QUESTION PAPERS



FORM 2 HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI
TEN QUESTION PAPERS

Prefer Calling Amobi Group of Examiners

@ 0743 333 000 OR 0706 851 439

For Marking Schemes

N/B In Response to the Huge Costs Associated in Coming Up with Such/Similar Resources Regularly, We inform us All, MARKING SCHEMES ARE NOT FREE OF CHARGE. However Similar QUESTIONS, Inform of soft Copies, are Absolutely FREE to Anybody/Everybody. Hence NOT FOR SALE

by Amobi Group of Examiners.


CALL AMOBI GROUP OF EXAMINERS @ 0743 333 000 OR 0706 851 439 TO ACQUIRE :













FORM TWO HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 01

UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Ponografia ni tendo, maandishi, picha au michoro inaoonyesha au kueleza uchi wa mtu au vitendo vya ngono kwa ajili ya kuchochea ashiki ya kuifanya. Mambo haya machafu huwasilishwa ana kwa ana kupitia sinema, magazeti, vitabu, muziki, televisheni, tovuti na kanda za kunasia picha na sauti. Ponografia imekuwepo tangu jadi, hasa katika nchi za magharibi. Lakini sasa limekuwa tatizo sugu. Hii ni kwa sababu imeenea kote ulimwenguni mithili ya moto mbugani wakati wa kiangazi. Kuenea kwake kumechangiwa na mambo kdha wa kadha. Mchango mkubwa zaidi ukiwa umetokana na kuimarika kwa vyombo vya teknologia ya habari na mawasiliano. Hata hivyo, kazi hii hubuniwa au kuchukiza wanajamii waadilifu. Kundi lingine ni lile la wanaochukia ponografia kama nyenzo ya kutosheleza ashiki zao. Kwa mfano, baadhi ya wanamuziki hutumia ponografia kuvutia wateja na hivyo kuzidisha mauzo yao.

Kushamiri kwa wimbi na uonyeshaji wa ponografia kuna athari kubwa kwa jamii hasa watoto.Ingawa watu wengine hudai picha hizi haziwathiri, upo ushahidi kuonyesha kuwa wale wanaotazama picha za ngono hupata matatizo. Lazima ieleweke kwamba kinachoonekana kwa jicho au kusikika kwa sikio huathiri fikira au hisia. Picha za matusi zinachangia kwa kiasi kukubwa kuharibu akili. Badala ya kuzingatia mambo muhimu kama vile masomo, watu huanza kutafakari mambo machafu.

Vijana wengi ni kama bendera, huyaiga wanayoyaona na kuyasikia. Hili ni tatizo linalowafanya kuacha mkondo wa maadili. Hivyo basi wengi hushawishiwa kuingilia shughuli za ngono mapema kabla hawajakomaa kimwili, kiakili na kihisia. Matokea yake ni ukahaba, utendaji mbaya shuleni, mahudhurio mabaya ya darasani na mimba zisizotarajiwa. Vijana wengi huacha shule kabisa huku wengine wakiambukizwa magonjwa ya zinaa ambayo yanaweza kuwaletea mauti.

Yasemekana kuwa akili za binadamu hunasa zaidi mambo yanayowalishwa kwa picha na hivyo basi matusi haya yaweza kudumishwa katika kumbukumbu zao. Tabia mbaya kama vile ushoga, ubasha na usagaji huwa matokeo yake na hata matokeo ya vijana hugeuka wanapoanza kuiga mitindo mibaya ya mavazi yanayoanika uchi wao. Hali kadhalika, lugha, ishara na miondoko inayohusiana na ngono huibuka. Yote haya yanakinzana nadesturi za desturi za mwafrika. Si ajabu visa vya ubakaji vinaongezeka kuchapo. Utazamaji wa picha chafu aghalabu huandamana na maovu mengine kama vile unywaji pombe na matumizi ya vileo ambavyo huchochea uchu wa ngono na kuibua tabia za kinyama.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Kuendelea kuzitazama picha hizi huzifanya nishai na hisia za watu kuwa butu, huondoa makali kiasi kwamba hata katika uzima mtu hupoteza mhemko na kugeuzwa kuwa mtegemezi wa ponografia. Tatizo hili linaenea kwa vishindo mjini na vijini. Ipo haja ya dharura kuikinga jamii kutokana na malezi haya yasiyo na kizuizi.

Kuongeza ufahamu wa umma wote kuhusu uovu wa picha hizi, watu kuwajibika kwa kuwalinda na kuwahimiza vijana kuhusu maovu haya na wale wenye midahilishi, video na sinema kutowaruhusu vijana kutazama uchafu huu kunaweza kuwa maana ya kuyakinga au hata kuyaepuka madhara ya ponografia. Ni sharti pia sheria izuie na kupiga marufuku utengenezaji na ueneaji wa upungufu huu. Bila shaka, sheria na hatua kali ziweze kuchukuliwa dhidi ya waivunjao. Hali kadhalika, wazazi wasijipweteke tu bali wawaelekeze watoto wao ipasavyo na kila mtu alitekeleze jukumu lake.

MASWALI

a) Yape makala uliyosoma anwani mwafaka **(al 1)**

b) Toa sababu za kusambaa kwa uchafu unaozungumziwa katika taarifa. **(al 2)**

c) "Bendera hufuata upepo" Thibitisha ukweli wa kauli hii kulingana na makala **(al 1)**

d) Ponografia huchangia madhara mengi hasa miongoni mwa vijana. Taja manne. **(al 4)**

e) Ni hatua zipi zinazofaa kuchukuliwa dhidi ya aina ya uozo unaozungumziwa na mwandishi? **(al 4)**

f) Fafanua msamiati huu kimuktadha.

i) Uchu

ii) Wasijipweteke

iii) Kuwa butu

MATUMIZI YA LUGHA(AL 55)

a i) Sauti ni nini katika lugha **(al 1)**

ii) Taja sifa mbili bainifu za /m/ **(al 2)**

b) Kwa kutoa mifano, eleza dhana hizi: **(al 2)**

i) Silabi wazi

ii) Silabi funge

c) Ainisha mofimu katika neno : **(al 3)**

Anatupikia

d) Bainisha aina za nomino zilizotumika katika sentensi ifuatayo.

i) Juma alimpa mtoto yule maji ya Baraka **(al 4)**

e) Andika kwa wingi:

i) Ile ya kujengea haijaletwa

ii) Andika kwa umoja

Mishale yao ilifungwa kwa manyoya mengi meusi **(al 2)**

f) Andika katika ukubwa wingi

Njia hii inafaa zaidi kuliko ile **(al 2)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

g) Yakinisha:

i) Sikusikia kuwa alichapwa wala kuumizwa **(al 2)**

ii) Asingefika mapema asingemsaidia **(al 2)**

h) Taja ngeli za nomino zifuatazo **(al 3)**

i) Maziwa

ii) Chai

iii) Kinyongo

i) Tofautisha maana katika sentensi zifuatazo:

i) Chakula chote kinapendeza

(ii) Chakula chochote kinapendeza

j) Tumia neno "alasiri"katika sentensi kama: **(al 2)**

i) Nomino

ii) Kielezi

k) Kirai ni nini? **(al 2)**

l) Wachezaji walikula chakula chote.

Anza: Chakula

m) Tambua aina ya maneno :

i) Ng'ombe mweusi atachinjwa leo **(al 2)**

n) Kwa kutoa mifano, eleza maneo mawili ya Ritifaa

o) Eleza maana ya: **(al 2)**

i) Ala tuli

ii) Ala sogezi

p) Bainisha matumizi ya kiambishi 'ni' katika sentensi hizi:-

i) Alikula shuleni

ii) Ni mchezo huo

q) Andika sentensi zifuatazo ukizingatia maagizo uliyopewa katika mabano. **(al 2)**

i) Magari yote yalitiwa vidhibiti mwendo (Mazoea)

ii) Alichora na akatuzwa (hali timilifu)

r) Kamilisha methali zifuatazo **(al 2)**

i) Ziniwi likujualo……

ii) …..……..…… Hafikilii mbingu

s) Toa maana mbili ya sentensi hii:-

Babu alinipigia mpira **(al 2)**

t) Eleza maana ya misemo hii **(al 2)**

i) Valia miwani **ii)** Kula kadhongo

u) Huku ukitoa mifano, eleza maana ya viambishi awali na viambishi tamati. **(al 4)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

ISIMU JAMII **(AL 12)**

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.

Jane:Hallo John
John:Hallo Jane
Jane: Uko wapi
John:Niko kazini
Jane: Umelost hivi kwa nini?
John:Kazi mob tu na…….
Jane: Tukutane wapi.....lini?
John:Hallo…..hallo

a) Tambulisha muktadha wa mazungumzo haya. **(al 2)**
b) Taja sifa zozote nne zinazotambulisha mazungumzo haya. **(al 8)**

FASIHI SIMULIZI **(AL 20)**

1) Eleza sifa za hadithi. **(al 5)**
2) Taja sifa tano za mtambaji bora. **(al 5)**
3) Eleza umuhimu wa vitunza-ndini . **(al 5)**
4. Eleza kikamilifu umuhimu was fasihi simulizi katika jamii. **(al 5)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM TWO HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 02

ALAMA 20

1 Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya: "……. siku hiyo nilirudi nyumbani nikiwa nimesikitika na kujawa na majonzi tele. Nilikuwa sijawahi kuona ajali mbaya kama hiyo"

B UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma taarifa hii kisha ujibu maswali ifuatayo.

Ukandaji

Je,unajua kuwa ukandaji wa mwili umetumika kama njia mojawapo ya matibabu toka dahari? Watu wanaofahamika kutumia ukandaji kimatibabu toka jadi ni Wahindi,Wachina,Wagiriki,Warumi na Waafrika.

Ukandaji unajulikana kuwa na manufaa makubwa kimatibabu. Mathalani,ukandaji hufungua vitundu vya ngozi. Ufunguzi huu huondoa sumu mwilini kupitia kwa utoaji jasho. Pili,ukandaji hupunguza mkazo wa misuli. Misuli ikiwa na mkazo zaidi kwa muda mrefu huleta urundikaji wa asidi. Ukandaji huondoa asidi hii,huufanya mwili kuwa mlegevu,humletea mtu uchangamfu na kuondoa uchovu.

Halikadhalika,ukandaji huimarisha mzunguko wa damu mwilini kwa wepesi. Hali hii huhakikisha kuwa virutubishi vya mwili huweza kufikia viungo vyote vya mwili. Hili nalo huchangia kuzidisha uwezo wa mwili kujikinga na maradhi. Hewa safi ya oksijeni huweza pia kusambaa kote mwilini kupitia kwa uimarishaji wa mzunguko wa damu. Aidha,ukandaji wa taratibu na polepole hupunguza mkazo wa neva na kuziliwaza ukandaji wa kasi huchangamsha neva na kuimarisha utendaji kazi wake.

Ukandaji unaweza kufanyiwa kiungo chochote mwili ni. Ukandaji huu huweza kuwa na matokeo mbalimbali mwilini.

Mathalani,ukandaji wa njia ya chakula mwilini,hasa tumbo na utumbo,huimarisha usagaji wa chakula na kuchangia uondoaji wa uchafu na sumu mwilini. Nao ukandaji wa njia ya mkonjo hustawisha uondoaji wa chembechembe za sumu mwilini.

Kwa kawaida,viganja vya mikono hutumika katika ukandaji. Viungo hivi vinapaswa kuwa na wororo. Wororo huu hupatikana kwa kutumia mafuta. Mafuta ambayo ni bora zaidi kwa shughuli za ukandaji ni ya ufuta au simsim. Matumizi ya kitu chochote kama ungaunga kinachoweza kuziba vitundu vya ngozi hayapendekezwi.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Ukandaji wapaswa kutekelezwa kwa njia ifuatayo. Mtu aanzie mikono na miguu. Kisha aingie kukanda kifua,tumbo,mgongo na makalio. Hatimaye,akande uso na kichwa. Mtu anaweza kutumia kitambaa kukandia mgongo. Ni bora kutumia viganja vya mikono kukandia. Kwa njia hii,manufaa huwa maradufu. Kwanza,tutanufaika na ukandaji na wakati huo huo tutakuwa tukifanya mazoezi ya viungo. Wasioweza kujikanda,wanaweza kuomba msaada. Ni muhimu ukandaji ufuatiwe na kuoga kwa maji vuguvugu.

Kwa walio na tatizo la shinikizo au mpumuko wa damu wanaweza kubadilisha utaratibu wa ukandaji. Waanzie kichwani,kisha waelekee usoni,kifuani,tumboni,mgongoni,makalioni,miguuni na kuhitimisha mikononi.

Hata hivyo,ukandaji haupaswi kufanywa wakati mtu anaugua maradhi yoyote. Wanawake wajawazito nao wanatakiwa kuepuka ukandaji wa tumbo. Halikadhalika,ukandaji wa tumbo hauruhusiwi wakati mtu anaendesha,ana vidonda vya tumbo au uvimbe tumboni. Hatimaye,ukandaji haupendekezwi iwapo mtu ana maradhi ya ngozi.

MASWALI

(a) Ukandaji ni nini? **(alm 1)**

(b) Eleza manufaa matatu ya ukandaji. **(Alm3)**

(c) Ukandaji unatakiwa kutekelezwa kwa njia gani? **(alm2)**

(d) Ukandaji unatakiwa kutekelezwa na nani na kwa nini? **(alm2)**

(e) Onyesha ni lini ukandaji haupendekezwi. **(alm2)**

(f) Eleza maneno yafuatayo kama yalivyotumika: **(alm5)**

(i) ufunguzi

(ii) auni

(iii) maradufu

(iv) maji vuguvugu

(v) shinikizo la damu

(C) UFUPISHO

Soma taarifa hii kasha ujibu maswali

Kuna wataalamu siku hizi wanaosema kuwa jela si pahala pa adhabu bali pa matibabu. Yaani madhumuni ya kumtia mhalifu jela isiwe kumwadhibu kwa makosa aliyofanya bali iwe kumtibu na kujaribu kumrekebisha tabia yake ili awe raia mwema.

Zamani wahalifu waliadhibiwa kwa mujibu wa makosa waliyoyafanya. Mhalifu aliyefanya makosa madogo madogo alifungwa lakini mtu aliyeua naye aliuawa. Sasa wataalamu wanatuambia kuwa mhalifu akiadhibiwa anapokuwa kifunguno,basi akitoka hurejea tena kufanya uhalifu. Madhumuni ya kumtia jela iwe si kumwadhibu bali kumfunza tabia njema. Wanatuambia

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

kuwa makosa afanyayo mhalifu yanatokana na matatizo ya jamii kwa jumla,nayo ni matatizo kama ya umaskini, msongamano wa watu,kosa afanyalo mhalifu si kosa lake pekee bali ni kosa la jamii nzima.

Jitu lilizoea kuua halioni kitu kumpiga mtarimbo au rungu la kichwa na kumyang'anya kila alicho nacho. Siku hizi,jitu kama hili baadhi ya wataalamu husema lisiuawe lifungwe maisha tu. Lakini 'kifungo cha maisha' ni kama tunavyokijua. Muuaji hufungwa pengine miaka kumi tu kisha husamehewa muda uliobaki. Hapo tena huwa huru ama kuifichua mali aliyoiiba na kuistarehea raha mustarehe au kurejea tena kufanya uhalifu.

Haya ni kinyume kabisa na mambo yaliyokuwa zamani. Aliyeua aliuawa kwa hivyo watu waliogopa kuua. Raia na pia askari waliokuwa wakiwasaka wahalifu walinusurika vifo kwani wahalifu wengine walichukua silaha za hatari kama bastola na bunduki.

Sasa wale wahalifu wabaya sana – mijizi, minyang'anyi na wauaji ndio wanaotukuzwa. Magazeti huwashawishi makatili hawa na kuwapa mapesa chungu nzima waeleze maisha yao ya kikatili. Magazeti haya sasa ndiyo yanayopata wasomaji wengi. Pia wachapishaji vitabu vya hadithi zinazohusikia na uhalifu, biashara zao zinazidi kustawi. Kadhalika sinema zinazoonyesha picha za ukatili; wizi na mauji hujaa watazamaji wanaoshangilia uhalifu ufanywao.

Wahalifu kwa upande mmoja wanatukuzwa na masinema vitabu na magazeti na kwa upande mwingine "haki" zao zinapiganiwa na baadhi ya wataalamu. Watu wanaowalaani wahalifu ni wale waliohasirika tu na kuteswa na wahalifu . Baadhi yao hata kulaani hawawezi kwa sababu wameshauawa,hawana tena kauli.

MASWALI

(a) Fupisha aya ya kwanza hadi ya tatu kwa maneno 50.

Matayarisho

Nakala safi **(alama 6/mtiririko 2)**

(b) Fupisha aya mbili za mwisho kwa maneno kati ya 45-50

Matayarisho

Nakala safi **(alama 6/Mtiririko 1)**

D MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40)

(a) Eleza tofauti kati ya sauti /z/ na /d/ **(ala 1)**

(b) Eleza tofauti kati ya:

(i) Mofimu huru

(ii) Mofimu tegemezi **(ala 2)**

(c) Ainisha viambishi katika sentensi hii.

(i) Mlipewa **(ala 2)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

(d) Onyesha kundi nomino na kundi tenzi katika sentensi hii.

(i) Nyayo za wanyama hao zimeonekana hapa. **(ala 2)**

e) Onyesha nomino za jamii katika sentensi zifuatazo

(i) Chuki baina ya jamii lazima ikomeshwe barani Afrika.

(ii) Wageni watatumbuizwa na bengi ya kayamba Afrika.

f) Bainisha vitenzi halisi kwa kuvipigia mstari

(i) Nyanchama hakufika mkutanoni

(ii) Horukut amerudi kutoka masoni **(ala 2)**

g) Eleza maana ya misemo ifuatayo.

(i) kupiga domo

(ii) kupiga kijembe **(ala 2)**

h) Tunga sentensi mbili kuonyesha tofauti kati ya maneno haya.

(i) shuka

(ii) suka **(ala 2)**

(i) Onyesha vivumishi vya sifa katika sentensi zifuatazo.

(I)(i) Anayetaka chakula kitamu ni nani?

(ii) Kiatu kirefu kimeng'oka kikanyagio. **(ala 2)**

(j) Geuza neno lililopigwa mstari kuwa kiwakilishi

(i) Mtoto <u>mbaya</u> aliadhibiwa **(ala 1)**

(k) Yakinisha sentensi ifuatayo katika umoja.

(i) Nyuzi zisingekatika zisingepotea **(ala 2)**

(l) Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatavyo.

(i) Nafsi viambata

(II) Visisitizi

m) Tumia kiwakifishi kifuatacho kubainisha matumizi yake katika sentensi ili kutoa maana mbili tofauti.

(i) Ritifaa **(ala 4)**

n) Andika katika udogo na wingi

(i) Njusi aliyekuwa na jicho moja alianguka mtoni **(ala 2)**

(o) Taja visawe vya maneno yafuatayo.

(i) Damu

(ii) Mjinga

q) Andika sentensi hii katika ukubwa

(i) Huyo nyoka alikatwa mkia na mvulana yule **(ala 2)**

r) Tumia kitenzi jina na kivumishi kutunga sentensi **(ala 2)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

s) Nyambua

Filisisha (tenda) **(ala 1)**

t) Sahihisha:

Kwenye nilisomea ni bali **(ala 1)**

u) Tumia herufi mwafaka kuainisha maneno katika sentensi hii.

(i) Ingawa anataka kucheza karata,ni mlevi **(ala 3)**

E. ISIMU – JAMII

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Mhudumu: Mnakaribishwa. Menyu hii hapa.

Mtakula nini?

Mteja 1: Naomba uniletee mix na ugali. Fanya haraka.

Mteja 2: Mhudumu,hebu leta madodo na chemsha mbili. Pia niletee maji ya machungwa.

Mhudumu: Sawa. Baada ya dakika moja utapata yote uliyoagiza.

Mteja 1: (Akila) Wewe-Please bring me drinking water. Yawe baridi tafadhali.

Mhudumu: Ndiyo haya hapa mezani. Glasi ndio hii pia,karibu.

Mteja 2: Nina haraka mzee. Wapi tooth pick?

Mhudumu: Hizo hapo ,mezani karibu na maji.

Mteja 1: (Akiita) Mhudumu,naomba uniletee ugali saucer tafadhali.

Mhudumu: Naam.

Mteja 2: (Akisimama) Nimeshiba. Hizi hapa pesa

Niletee change haraka niondoke.

MASWALI

a) Ni sajili gani inayohusishwa katika mazungumzo haya? **(ala 2)**

b) Taja sifa zozote tano za sajili hii **(ala 5)**

c) Dondoa msamiati unaotambulisha sajili hii **(ala 3)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM TWO HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 03

1. UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Changamoto kubwa inayowakabili watu wengi katika mataifa yanayoendelea ni suala la chakula. Suala hili linaweza kuangaliwa katika sawia mbili tofauti. Kuna tatizo linalofungamana na uhaba wa chakula chenyewe. Uhaba huu unaweza kutokana na utegemezi mkubwa kwa zaraa kama nyenzo kuu ya uzalishaji wa chakula.

Zaraa katika mataifa mengi hususan yanayoendelea, hutegemea mvua. Kupatikana kwa mvua huathiriwa na mabadiliko ya tabianchi ulimwnguni. Matendo na amali za watu kama ukataji wa miti na uchafuzi wa mazingira huwa na athari hasi kwenye tabianchi hiyo. Mabadiliko ya tabianchi huweza kuvyaza ukama kutokana na **ngambi ya mvua**.

Kibinimethali kutokea wakati mafuriko yanapotokea na labda kuyasomba mazao mashambani na kusababisha baa la njaa. Hali hizi mbili husababisha matatizo makubwa ya chakula na kuathiri pakubwa suala zima la usalama wa chakula. Ili kuzuia uwezokano wa kuwepo kwa shida hii, pana haja ya kuwepo kwa mikakati na sera za kuhakikisha kuna usalama wa chakula. Kwa mfano, pana haja ya kukuza kilimo cha umwagiliaji ili kuepuka **adha** inayosababishwa na ukosefu wa mvua. Kwa upande mwingine, sharti zichukuliwe hatua mufidi za kuzuia na kupambana na athari za gharika.

Changamoto nyingine inahusiana na usalama wa chakula chenyewe. Chakula kilichosibikwa na vijasumu au kwa njia nyingine ile huweza kumdhuru anayehusika. Msibiko wa chakula unatokana na vyanzo tofauti. Mathalan uandalizi wa chakula kilichochafuliwa na choo, kutozingatia mbeko za usafi, uandaaji wa chakula na kukiweka katika hali ya uvuguvugu kabla ya kukipakua – hali inayochochea ukuaji wa viini na ulaji wa chakula kisichoandaliwa vyema.

Ili kuepuka uwezekano wa kuathirika, pana haja ya kuzingatia usafi wa chakula na uandalizi unaofaa. Fauka ya hayo, vyombo cya uandalizi view safi, kanuni za usafi zifuatwe, upikaji na uandaaji uwe kamilifu. Hali hii isipozingatiwa, siha za raia wenyewe zitaathirika pakubwa.

Maswali.

1. Taja aina mbili za kuangalia suala la chakula katika mataifa yanayoendelea. **(ala 2)**

2. Taja hatua mbili zinazoweza kuchukuliwa kupambana na tatizo la chakula. **(alm 2)**

3. Eleza jinsi nne tofauti namna chakula kinavyoweza kuwa si salama? **(alm 4)**

4. Kwa nini ni rahisi kukipakua chakula baada ya kukiandaa tu? **(alm 1)**

5. Ni mapendekezo gani anayoyatoa mwandishi kuhakikisha kuwa chakula kinafaa? **(alm 4)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

MATUMIZI YA LUGHA

1. Kwa kutoa mifano eleza tofauti kati ya**:** **(alm 2)**

i. Silabi funge **ii.** Silabi wazi

2. Onyesha sauti zenye sifa zifuatazo**:** **(alm 2)**

i. Kipasuo cha ufizi **ii.** Kikwamizo cha kaakaa laini

3. Tambua aina ya nomino katika sentensi zifuatazo**.** **(alm 2)**

i. Mchanga hufanya miti kumea.

4. Bainisha mofimu katika kitenzi**.** **(alm 2)**

Kilipikika

5. Tambua vivumishi katika sentensi ifuatayo na ueleze ni vya aina gani**.** **(alm 2)**

i. Mtoto wake ameng'oka jino. **ii.** Msemo wenye tafsida hupendwa.

6. Andika kinyume cha: **(alm 1)**

Tulinunua nguo aliizozianika jana.

7. Nomino 'uki' iko kwenye ngeli gani. **(alm 1)**

8. Ainisha vitenzi kwenye fungo zifuatazo: **(alm 3)**

i. Yatakuwa yangali yanakoma. **ii.** Maria na Atieno ni wanafunzi watiifu.

9. Onyesha vielezi katika sentensi zifuatazo. **(alm 2)**

i. Rais ametutembelea mara sita mwaka huu. **ii.** Nendeni haraka shuleni.

10. Eleza maana inayojitokeza kwenye sentensi ifuatayo. **(alm 1)**

i. Waiteni watu wale.

11. Tumia kiwakilishi kisisitizi kutungia sentensi ya wingi wakati uliopita. **(alm 2)**

ISIMU JAMII

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Haya ng'ara … Ng'ara leo! Nguo motomoto. Ng'ara leo kwa bei rahisi. Hamsini hamsini shati. Kuona ni bure. Bure kwa bure. Shika mwenyewe ujionee. Bei nafuu. Bei ya starehe. Haya, haya. Usikose mwanangu! Hamsa! Hamsa! Fifty!Hamsa! Fifty! Hamsa na nyingine.

Maswali.

a. Bainisha sajili ya mazungumzo haya. **(alm 1)**

b. Eleza sifa nane za sajili hii kwa kurejelea kifungu hiki. **(alm 4)**

FASIHI SIMULIZI.

a. Fafanua maigizo. **(alm 2)**

b. Ainisha kipera cha maigizo. **(alm 4)**

c. Eleza sifa za maigizo. **(alm 4)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM TWO HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 04

SEHEMU A; INSHA ALAMA 20

Andika ratiba ya siku ya wazazi shuleni

SEHEMU YA B: UFAHAMU: (ALAMA 15)

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

MAVAZI REKEBISHENI

Vazi njema kivaliwa, huongezeka heshima,
Staha mtu kapewa, poteendapo daima,
Mavazi duni si sawa, kina dada ninasema,
Mavazi rekebisheniusheratiumezidi.

Longi kwa nyuma kushika, na mapajani kubana,
Chupizilipowafika, dhahiri kuonekana,
Buremunaaibika, na kujishusha maana,
Mavazi rekebisheni, usheratiumezidi.

Kifuanikujikaza, maziwayaning'inie,
Kitu gani munawaza, hamna bahari nyie,
Ni ashikimwasambaza, sikizeniniwambie,
Mavazi rekebisheni, usheratiumezidi.

Msichana ni hatia, magotinikufichuka,
Hivyo basi kuvalia, rindalisoyafunika,
Huenda zusha hisia, maovuyakawafika,
Mavazi rekebisheni, usheratiumezidi.

Sitakosakuzitaja, skatimnazovaa,
Zaisha kwa mapaja, kikirikuchuchumaa,
Iko wazi nyonga moja, mkatoulivyokaa,
Mavazi rekebisheni, usheratilumezidi.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Wazi nitawasomea, nguo hizi nguo gani?
Dada zetumwakosea, kuzivaahadharani,
Ndizo hizo huchochea, usherati mitaani,
Mavazi rekebisheni, usheratiumezidi.

Nguo chini zishusheni, mwilini mzipanue,
Heri kuingia deni, za heshima mnunue,
Kuigiza za kigeni, ni utumwamtambue,
Mavazi rekebisheni, usheratiumezidi.

Betitisanamaliza, kalamunaweka chini,
Iwapo wajiuliza, nakereketwa ni nini?
Ni stahanahimiza, sio wake kuhaini,
Mavazi rekebisheni, usheratiumezidi.

MASWALI YA USHAIRI

(a) Shairi hili ni la aina gani? **(alm 2)**
(b) Eleza vina vya beti za kwanza mbili **(alm 2)**
(c) Toa kibwagizo cha shairi hili kisha ufafanue maana yake. **(alm 2)**
(d) Eleza maana ya misamiati hii kama ilivyotumika katika ushairi. **(alm 4)**

Staha –
Dhahiri –
Shani –
Duni –

(e) Shairi hili liko katika bahari zipi? **(alm 2)**
(f) Uhuru wa mshairiunadhihirikavipi katika shairi hili? **(Alm3)**

MATUMIZI YA LUGHA (AL 30)

1. Pambanua sauti hizi kama ni ghuna au si ghuna. **(al 1)**

/Z/ /K/

2. Eleza maana ya kiimbo. **(al 1)**
3. Eleza maana ya shadda. **(al 1)**
4. Eleza maana ya mofimu. **(al 2)**
5. Andika kwa wingi sentensi hizi. **(Al.2)**

i.Goti la mtoto liliumia.
ii. Ukwato wa ngamia ni mpana.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

6. Bainisha nomino hizi ni za aina gani. **(al.2)**

i.Sukari. **ii.**Mapenzi

7. Tumiavivumishi vya sifa katika mabanokukamilisha sentensi zifuatazo**.** **(al 2)**

i. Mtoto Yule ni _____ (nene)

ii. Bei ya meli ni _____ mno (ghali)

8. Jazapengo kwa kiulizi sahihi kisha uandike sentensi kwa wingi **(al 2)**

Ni mpishi _____ aliyepika.

9. Fafanua maana ya misemo ifuatayo. **(al2)**

i.Kula mate.

10. Andika katika ukubwa. **(al 2)**

i. Jiji hili litapanukaupesi. **ii.** Jizeelililokosa adabu limekaripiwa.

11. Geuza sentensi zifuatazo katika hali ya usemi halisi. **(al 2)**

i. Ruhenialishauliwa na kasisiaache tabia mbaya.

ii. Mwalimu alimwabiapremjiafanye bidii katika masomo yake.

12. Andika vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendeshana. **(al 2)**

i.Penda .

ii. Endesha.

13. Tambua kikundi nomino (KN) na kikundi tenzi (KT) katika sentensi zifuatazo. **(al 2)**

i. Anatembea kwa madaa kama tausi.

14. Kanusha sentensi zifuatazo. **(Al 2)**

i. Mimi nilicheza. **ii.** Wewe huchora.

15. Kamilisha methali zifuatazo ? **(al 1)**

i. Cha kuvunda. _____

16. Andika kinyume cha maneno yafuatayo. **(al 2)**

i. Tandika _____

ii. Umba _____

17. Pambanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mstari. **(al 2)**

Naimba huku nafanya kazi. _____

ISIMU JAMII(ALAMA 5)

Eleza sifa za lugha ya hotelini

FASIHI SIMULIZI (al 10)

a) Taja aina nne za hadithi.

b) Eleza umuhimu wa hadithi.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM TWO HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 05

UFAHAMU: (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali:

Takwimu zilizothibitishwa zaonyesha kuwa kila sekunde nane mtu mmoja hufa duniani kutokana na utumiaji wa tumbako. Kwa siku basi, watu 10,800 hufa. Wengi wa wavuta sigara huanza katika umri kati ya miaka kumi na mitatu hadi kumi na tisa. Takwimu zaonyesha kuwa mtu akivuta sigara kwa zaidi ya miaka ishirini huupunguza umri wake kwa kati ya miaka 20 hadi 25 zaidi ya ambaye hajawahi kuvuta. Hii ni kwa kuwa tumbako ina zaidi ya kemikali 4,000 zinazodhuru afya.

Mojawapo ya madhara makuu zaidi yanayosababishwa na sigara ni saratani. Kunayo saratani ya ngozi – vidonda visivyopona huchubuka ngozini na baada ya muda hugeuka na kuwa kansa. Iri ya mapafu hutokea vifuko vya hewa vinapopasuka na hivyo kutatiza uvutaji wa oksijeni na utoaji wa kabondayoksaidi. Moshi pia husababisha madhara kwa njia ya kupitisha hewa, yaani umio, ambapo njia hii yaweza hata kuzibika hivyo kulazimu tundu kutobolewa kooni ili mgonjwa aweze kupumua. Kabla ya kufika kooni na mapafuni, moshi hupitia mdomoni. Saratani ya mdomo na ulimi basi hupatikana zaidi miongoni mwa wavuta sigara. Pia kidonda chochote, kwa mfano baada ya kung'olewa jino, huwa vigumu kupona kwa mvutaji sigara.

Kwa wanawake, kuna hatari ya kupatwa na iri ya fuko la uzazi. Madhara kwenye njia nzima ya uzazi huifanya iwe vigumu kwa wanawake wavuta sigara kuhimili. Ni rahisi pia kuzaa njiti. Mtoto wa mvutaji huzaliwa akiwa mwepesi zaidi ya kawaida. Hii husababishwa na kabonimonoksaidi kutoka kwa sigara inayomdhuru mtoto tumboni. Saratani hii husababisha hata kifo cha mtoto aliye tumboni. Wengine wazaliwapo huwa na hatari ya kupatwa na saratani zaidi ya waliozaliwa na akina mama wasiovuta sigara.

Aina zaidi za saratani zinazowakumba wavuta sigara ni kama vile saratani ya pua, ya tumbo, ya figo, ya kibofu cha mkojo, ya kongosho, ya njia ya kinyesi na hata saratani ya matiti inayowaathiri zaidi wanawake.

Shida za sigara sio saratani pekee; sigara husababisha shida za macho na masikio kwa kiasi kikubwa. Mboni ya jicho yaweza kufunikwa na utando, hali inayoweza kusababisha hata upofu. Macho yaweza kuwashwa na moshi mkali wa sigara au mishipa ya macho iathirike na kemikali zinazofika kwayo kupitia kwa mishipa mapafu yanapoathirika. Masikio nayo huathiriwa na uchafu wa tumbako unaoganda kwenye mishipa hadi sehemu za ndani za masikio. Damu hupunguza mwendo ufaao masikioni hivyo yanaugua. Moshi na kemikali za tumbako pia hujeruhi sehemu za

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

ndani na athari hii yaweza kuenea hadi ubongoni na kusababisha utando unaofunika ubongo. Hali hizi zaweza kusababisha uziwi.
Mifupa na meno huathirika pia. Mifupa huwa myepesi, hukosa nguvu na kuwa rahisi kuvunjika. Mvuta sigara akivunjika mfupa huchukua muda wa asilimia themanini (80%) kupona zaidi ya mtu asiyevuta. Meno nayo hutatizika katika ukuaji wake kutokana na kugandwa na moshi wenye kemikali. Hali hii husababisha harufu mbaya, uchafu pamoja na kuoza kwa meno.
Ngozi ya mvuta sigara hukaushwa na kemikali kwa sahabu uwezo wake wa kujirekebisha na kujilainisha hupunguzwa pakubwa. Hali hii husababisha ukavu unaoonekana pamoja na makunyanzi yanayomfanya mvuta sigara aonekane mzee zaidi ya umri wake. Vidole navyo vilevile hugandwa na kutu ya sigara, nazo kucha na vidole hugeuka rangi vikawa vya manjano, hudhurungi au maji ya kunde. Vidole pia hukaushwa na moto na kemikali ya sigara. Nywele za mvuta sigara pia huathirika kwa kuwa kemikali huipunguza kinga ya mwili hivyo mizizi ya nywele kukosa nguvu. Nywele za mvuta sigara zaweza kung'oka mapema.
Sigara husababisha magonjwa ya moyo na vidonda vya tumbo. Kwa moyo, sigara husababisha shinikizo la damu na hatimaye mshtuko wa moyo waweza kutokea na kusababisha hata kifo. Kwa tumbo, sigara hupunguza uwezo wa kinga zake wa kuikinga dhidi ya asidi zinazosaga chakula. Pia hupunguza uwezo wa mwili wa kujikinga dhidi ya vidonda vya tumboni. Vidonda vya tumbo vya mvuta sigara huwa vigumu kupona na, ni rahisi kutokea tena baada ya kupona.
Kwa mwanamume, mpigo wa damu kwenye sehemu za uzazi huathiriwa. Hali hii ikizidi husababisha hata upungufu wa nguvu ya mbegu kwenye shahawa. Hata ugumba waweza kutokea. Pia watoto wa mwanamke mvuta sigara waweza kuzaliwa wakiwa na kasoro. Mimba zingine zilizotungwa na wanawake wavuta sigara pia hutunguka. Na si hayo tu; madhara ya sigara ni mengi zaidi.

Maswali

a) Yape makala haya kichwa. **(alm 2)**
b) Mbali na athari kwa uzazi kwa wanawake na wanaume na sura/umbo la binadamu, taja madhara mengine ya uvutaji sigara kwa binadamu**.** **(alm3)**
c) Kwa kurejelea kifungu onyesha kwamba sigara kwa wanawake hasa ni hatari mno. **(alm 4)**
(d) Je, ni kweli kuwa vifo vingi hutokea kwa sababu ya uvutaji sigara? Toa sababu. **(alm 2)**
(e) Eleza namna ambavyo uvutaji sigara huathiri sura ya mhusika. **(alm3)**
(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kwenye taarifa. **(alm 1)**
Gandwa _____

MATUMIZI YA LUGHA. AL 35

1. Eleza maana ya ishali zifuatazo. **(al 2)**
(i) Mofimu
(ii) Viambishi

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

2. Andika kwa wingi sentensi hii; **(al 1)**

(i) Goti la mtoto liliumia ————

3. Bainisha nomino hizi ni za aina gani. **(al 1)**

(i) Mzee

(ii) Oduori

4. Tumia vivumishi vya sifa katika mabano kukamilisha sentensi zifuatazo. **(al 2)**

(i) Mtoto yule ni ———————————— (nene)

(ii) Kiberiti si kifaa ———————————— kubeba. (zito)

5. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kuchaza viambishi vya upatanisho vya —ingine. **(al 2)**

(i) Mahali ————————————kulikobaki ni kwao.

(ii) Mwizi huyo ————————————hakupigwa risasi.

6. Ziandike upya sentensi zifuatazo ukitumia 'O'rejeshi. **(al 2)**

(i) Meno ambayo yanamuuma yatatiwa dawa. **(ii)**Kioo ambacho kilinunuliwa ni kipya.

7. Tambulisha vitenzi visaidizi katika sentensi hizi. **(al 2)**

(a) Hajaenda kusoma **(b)** Niliwahi kumweleza.

8. Sahihisha sentensi zifuatazo kimapokeo. **(al 2)**

(i) Zizi tuna sisi la ng'ombe kwetu.

(ii) Kiza cha abunuwasi kwenye kisa kinazikitisha.

9. Andika sentensi zifuatazo kwa wingi. **(al 2)**

(i) Nitaenda alasiri kumwangalia alikoenda.

(ii) Atamwinda mnyama huyo kisirisiri.

10. Tumia kihusishi kifaacho katika sentensi zifuatazo. **(al 3)**

(i) Amechuma matunda ————————rafiki yake

(ii) Walikimbia ————————swara.

(iii) Tutafanya kazi ————————wenzetu.

11. Tunga sentensi ukitumia vihisishi ukionyesha hisia zifuatazo. **(al 2)**

(i) Furaha. **(ii)** Dharau.

12. Andika kinyume cha vitenzi vifuatavyo**.** **(al 2)**

(i) Tandika **(ii)** Unga

13. Kamilisha methali zifuatazo. (al 2)

(i) Kawia——

(ii) Chovya chovya ——

(iii) Isipowasha————

(iv) Cha kuzama————

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

14. Kanusha sentensi zifuatazo. **(al 2)**

(i) Nilimwona akicheza

(ii) Ningalienda kwake ningalimpata.

15. Tambua kikundi Nomino na kikundi Tenzi katika sentensi zifuatazo. **(al 2)**

(i) Mwanafunzi amevaa sare safi mno

(ii) Sakafu ile inateleza sana

16. Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. **(al 2)**

"Njoo hapa" Asksri alimwita Juma.

17. Unda nomino mbili kutokana na kitenzi safari. **(al 2)**

18. Andika kitenzi kifuatacho katika kauli ya kutendeswa. **(al 1)**

Panga

FASIHI SIMULIZI AL 10

1. (a) Eleza maana ya methali **(al 2)**

(b) Fafanua sifa nne za methali **(al 8)**

ISIMU JAMII AL 10

1. (a) Eleza maana ya sajili ya bungeni. **(al 2)**

(b) Taja sifa nane za sajili ya bungeni. **(al 8)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM TWO HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 06

1. INSHA – ALAMA 20

"Wewe ni mwalimu mkuu wa shule yako. Andika hotuba utakayoitoa siku ya wazazi shuleni mwako."

UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali uliyoulizwa. (ala 15)

Mateso ya wanawakiwa ni suala la kijamii linalofaa kutazamwa kwa darubini kali. Hata hivyo wanoathirika zaidi ni watoto ambao bado wako katika umri unaohitaji kulelewa na kupewa mahitaji ya msingi kama mavazi, malazi, elimu na mengine anuwai. Hali ya kuachwa na wazazi imekuwa ikizikumba jamii tangu enzi za mababu na kila itokeapo, wanajamii huipokea kwa mitazamo tofautitofauti, hivyo kuwafanya wanawakiwa kuathirika sana.

Baadhi ya jamii zina imani za kijadi pamwe na mila zilizochakaa zinazozifanya kuamini kuwa baadhi ya vifo hutokana na laana. Wengine huchukulia kuwa mwendazake ameondolewa na ulogi. Imani kama hizi huifanya jamii kuwatia watoto waliochwa katika mkumbo ule ule, hivyo kuwaangalia kwa macho yasiyo ya kawaida. Hii husababisha dhana gande. Hali hii husababisha kuwachukulia watoto kama wanaotoka katika kizazi kilicholaaniwa. Jamii basi hukosa kuwapa watoto hawa stahiki yao. Hata wanapojitahidi kuiwania nafasi yao, waliowazunguka huwavunja mioyo. Jitihada zao huishia kuwa si chochote kwa kuwa jamii inawatazama kama waliolaaniwa.

Punde baada ya mzazi mmoja au wote wawili waendapo wasikorudi, inatarajiwa kwamba aliyeachiwa mtoto awe mzazi wake, mwanafamilia au jirani awajibike na kumtunza mwanamkiwa. Kunao kadha wa kadha wanaowajibika – nina wavulia kofia. Hata hivyo wengi hutelekeza jukumu hii walilopewa na Muumba. Si ajabu basi kuona kuwa idadi ya watoto wanaozurura mitaani inazidi kuongezeka kila uchao. Ukichunguza utakuta kuwa wengi wa watoto hawa ni waliopotelewa na wazazi wao. **Inakera** zaidi kugundua kuwa baadhi ya watoto hawa wana mzazi mmoja. Kwamba mke au mume wa mtu ameaga, au iwe kwamba mzazi mmoja alimza mtoto na kumwachia mwenzake mzigo wa ulezi, aliyeachiwa na jukumu la kumpa mwanawe mahitaji ya msingi. Machoni pa jalali, kila anayeupuuza wajibu huu ana hukumu yake siku ya kiama!

Ni haki ya kila mtoto kupata elimu. Katika katiba ya Kenya mathalan, elimu ya msingi, yaani kuanzia shule ya chekechea hadi kidato cha nne ni ya lazima. Tangu hapo hata hivyo, jamii zimekuwa zikiwanyima wanawakiwa wengi elimu. Kwamba kunao wachache wanaowaelimisha baadhi ya wanawakiwa ni kweli. Hata hivyo, wengine hukosa hata wa kuwapeleka katika shule ya

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

chekechea, hivyo kuishia kutojua hata kuandika majina yao. Mfikirie mtu katika karne ya 21 asiyejua kusoma wala kuandika! Nani ajuaye, huenda huyo mwanamkiwa asiyepelekwa shuleni ndiye angalikuwa profesa, daktari, mwalimu, rubani au msomi mtajika na mtaalamu wa uwanja muhimu katika jamii!

Kila mtoto ana haki ya kulelewa hadi kufikia utu uzima kabla ya kupewa majukumu mazito. Katika katiba ya Kenya, utu uzima, ulio umri wa kuanza kufanya kazi huanzia miaka 18. Wanaohakikisha watoto hawa wametimiza utu uzima kabla ya kufanyizwa gange ngumu wanafaa pongezi. Hata hivyo wanawakiwa wamekuwa wakitumiwa na wengi kama punda wa huduma. Wanaaila wengine huwachukua wanawakiwa kwa machozi mengi wazazi wao waagapo na kuapa kuwahifadhi na kuwatunza wana wale wa ndugu zao, kumbe ni machozi ya simba kumlilia swara! Hata kabla ya mwili wa mzazi mhusika kuliwa na viwavi, mateso kwa mtoto yule huanza, akawa ndiye afanyaye kazi zote ngumu. Utakuta watoto wao wamekaa kama sultan bin jerehe huku mwanamkiwa yule akiwapikia, kuwafulia nguo, kudeki, karibu hata wa waoshe miili! Kazi kama zile za shokoa huwa za sulubu na aghalabu husindikizwa kwa matusi yasiyoandikika.

Baadhi ya **waja** walionyimwa huruma huwahadaa wanawakiwa na kuwapeleka ng'ambo wakitumia vyambo, kuwa wakifika kule watapata kazi za kifahari. Maskini wale huishia kushikwa shokoa, wakawa watumwa katika nyumba za waajiri wao, bila namna ya kujinasua. Wengine huishia kutumiwa kama watumwa wa 'Kimapenzi' katika madanguro, miili yao ikawa ya kuuziwa makahaba waroho wasiojali utu. **Kujinasua** kule huwa sawa na kujitahidi kuokoa ukuni uliokwishageuka jivu, maadamu wanawakiwa aghalabu hukosa watu wenye mioyo ya huruma ya kuwashughulikia. Wengi huitumia methali ' mwana wa ndugu kirugu mjukuu mwanangwa' kuwapuuzilia mbali wanawakiwa ambao hukimbiliwa tu wabinafsi hawa wanapofaidika wenyewe.

1. Kipe kifungu hiki kichwa mwafaka. **(ala.1)**

2. Eleza dhana ya 'Mwanamkiwa. **(ala. 1)**

3. Ni kategoria gani ya wanawakiwa inayosumbuka sana? **(ala. 2)**

4. Taja mambo mawili ambayo baadhi ya imani na mila za jadi huchukulia kuwa chanzo cha uanaukiwa. **(ala.1)**

5. Eleza kwa kifupi hali ya elimu ya wanawakiwa. **(ala.2)**

6. Taja mateso mawili ambayo wanawakiwa wanaoahidiwa kulepekwa ng'ambo hukumbana nayo. **(ala.2)**

7. Eleza unafiki wa baadhi ya watu wa jamii ya wanawakiwa. **(ala.3)**

8. Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala. **(ala.3)**

i) Inakela

ii) Waja

iii) Kujinasua

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

UFUPISHO

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali uliyoulizwa

Wanawake wanaoishi katika maeneo ya mashambani katika nchi zinazoendelea ni baadhi ya watu waliotopea na kubobea kwenye umaskini mkubwa na wanaoathiriwa na matatizo kwa kiwango kikubwa ulimwenguni. Jumla ya idadi ya wanawake hawa wanaoishi chini ya kiwango cha chini cha umaskini inakadiriwa kuwa zaidi ya milioni 600. Hii ni idadi kubwa hasa ikikumbukwa kuwa ni asilimia kubwa ya wanawake wanaoishi kwenye maeneo haya.

Ulimwengu umeshuhudia ongezeko la idadi ya watu au dadiwakazi; kuwako kwa matatizo ya kiuchumi ulimwenguni; mitafaruku na vita vya kikabila, majanga ya kiasilia kama mafuriko ya maji, ukame au milipuko ya volkeno katika maeneo yanayoathiriwa nayo. Sababu nyingine ni uharibifu na ushukaji wa hali ya kimazingira, mabadiliko ya desturi au thamani za kitamaduni; kusambaratika kwa familia au misingi ya familia; utengano na hasa wakati wa shida pamoja na uhamaji wa wanaume na kuwaachia jukumu kubwa. Aidha kuna kuongezeka kwa hali ya wanawake kuwa wazazi pekee na hivyo kuongeza idadi ya miji inayoongozwa na wanawake na kukosekana kwa mikakati bora au ifaayo ya kupambana na maisha.

Wanawake wanaoishi mashambani wanaathrika vibaya sana. Kwanza, kama masikini wanaishi katika mazingira makali. Pili, kama wanawake wanakabiliana na mapendeleo ya kisera na kitamaduni ambayo yanaudharau na kuupuuza mchango wao katika maendeleo. Tatu, kama viongozi wa miji (hasa wale wanaolea na kuzitunza jamaa zao peke yao) wanalazimika kupambana na uongozi wa miji pamoja uzalishaji. Aghalabu hawapati usaidizi au auni yoyote katika majukumu kama haya: wanalazimika kupambana nayo peke yao. Katika hali zote tatu zilizotangulia, wanawake hawapati nafasi zifaazo kushiriki katika maamuzi ya masuala yanayowahusu. Masuala mengi yanaamuliwa na wanaume bila ya kuwahusisha.

Licha ya dhiki yao kubwa, wanawake hawa wanachangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa njia tatu kuu. Mchango huu unaonekana katika kiwango cha jamii na taifa, kiwango cha mji na kupitia kwa kizazi kijacho. Katika kiwango cha kijamii na kitaifa, wanawake hawa ni chanzo cha nguvukazi. Nguvukazi hii inatokana na wao wenyewe pamojo na kizazi chao. Pia ni msingi muhimu wa uwekaji rasilmali na kuhifadhi; aghalabu wana uwezo bora wa kutunza chochote walicho nacho kuliko wanaume. Katika kiwango cha mji, wanawake wa mashambani wanahakikisha kuwako kwa chakula, na njia za kukitayarisha chakula hicho. Katika kiwango cha vizazi, wanawake hawa wanakuwa kiungo kikubwa kati ya kizazi kijacho na vizazi vya kesho. Hawa ndio wanaowatunza, kuwalea na kuwaelimisha watoto na kuhakikisha kuwa pana muungano kati ya vizazi vya jamii.

a) Ni sababu zipi zinazosababisha umaskini wa wanawake wa shambani? (Maneno 50 -55)

b) Eleza jinsi wanawake wa mashambani wanavyoathirika vibaya(maneno 40 – 45)

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Sarufi na matumizi ya lugha. (ala. 40)

a) Eleza sifa mbili za sauti|k|. **(ala.2)**

b) Andika mfano mmoja wa neno lenye muundo ufuatao: **(ala.1)**

IKII

c) Sentensi ambatano ni ipi? **(ala. 2)**

d) Unda sentensi yenye muundo ufuatao. **(ala.2)**

W+V+T+E

e) Onyesha viwakilishi (w) katika sentensi ifuatayo na ueleze ni vya aina gani. **(ala. 2)**

Wote walipewa kile kizuri.

f) Yakinisha sentensi ifuatayo. **(ala. 1)**

Hakula akashiba.

g) Kanusha sentensi ifuatayo. **(ala.2)**

Ningeenda kwake leo angenipa mawaidha.

h) Eleza dhana zinazojitokeza katika maneno yaliyopigiwa mstari. **(ala.3)**

a) Mtoto <u>mwenyewe</u> alianguka <u>mle</u>

b) Mtoto mwenye tabia nzuri ni Yule.

i) Tunga sentensi kuonyesha vielezi vifuatavyo. **(ala.3)**

a) Kielezi cha wakati

b) Kielezi cha mahali

c) Kielezi cha namna/jinsi

j) Andika katika msemo halisi. **(ala. 2)**

Rafiki yetu alitujulisha kuwa tungeondoka siku iliyofuatia kuelekea Afrika kusini.

k) Unda nomino kutokana na maneneo yafuatayo. **(ala. 3)**

Neno	Nomino
i) Fikiri	_____
ii) - la	
iii) kubwa	

l) Tunga sentensi moja moja kuonyesha aina zifuatazo za nomino. **(ala. 2)**

i) Nomino kitenzi – jina

ii) Nomino dhahania

m) Onyesha vivumishi (v) kwa kupigia mstari na ueleze ni vya aina gani. **(ala.2)**

Waziri wa kawi anaishi katika nyumba kubwa.

n) Tumia alama ya ritifaa katika sentensi kuonyesha matumizi mawili tofauti. **(ala. 2)**

o) Bainisha viambishii katika neno lifuatalo. **(ala.3)**

Waliotutenga

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

p) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizopewa. **(ala.6)**

Kitenzi	tendesha	tendeshea
Piga	_____	_____
-la	_____	_____
-nywa	_____	_____

q) Mahali palipotayarishwa pamejaa wageni kutoka mbali. (Anza kwa: wageni…) **(al.2)**

IV ISIMU – JAMII

Mtu X : wauza how much?
Mtu Y: Hamsini kastoma.
Mtu X: Kumbe ni expesive hivyo?
Mtu Y: Nitakupunguzia. Toa arobaini.
Mtu X: Haya. Nipatie change.

a) Hii ni sajili gani? **(ala.1)**
b) Eleza sifa tano za sajili hii. **(ala5)**
c) Taja athari mbili hasi za lugha ya 'Sheng' **(ala.2)**
d) Kwa nini vijana hutumia lugha ya 'Sheng' Eleza sababu mbili. **(ala.2)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM TWO HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 07

Insha ya kiuamilifu. (alama 20)

1. Hali ya usalama imekuwa ikizorota katika lokesheni yako.
Andika barua kwa chifu wa eneo lenu ukionyesha visa vya ukosefu wa usalama na upendekeze njia za kukabiliana na hali hiyo.

2.**UFAHAMU(AL.15)**

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

Aibu kubwa ya taifa kushindwa kukabiliana na tatizo sugu la ajali za barabarani bado inaendelea. Wahusika katika sekta ya uchukuzi na mawasiliano licha ya matumizi ya vidhibiti mwendo na kanda za usalama. Ajali za barabarani zinaangamiza idadi kubwa ya watu kila mwaka, wakiwemo viongozi na watu mashuhuri.

Miongoni mwa sababu ambazo zinaleta maafa barabarani ni pamoja na uendeshaji kasi kupita inavyotakikana, yaani kukiuka masharti yaliyowekwa na wizara ya uchukuzi na mawasiliano. Madereva wengi hung'oa vithibiti mwendo vilivyowekwa hawarekebishi mikanda ya usalama, wala hawa peleki magari yao kwa ukaguzi mara kwa mara kama inavyopaswa kutekeleza kanuni zilizowekwa kwa hivyo hutegemea hongo kuwa barabarani. Fauka ya hao, madereva wa malori na matrela mara nyingi huendesha magari hayo wakiwa walevi. Dawa za kulevya kama vile miraa na bangi, hutumiwa sana na watu hawa, na matokeo yake huwa ajali mbaya.

Hata hivyo, lawama haiwezi kuelekezewa madereva pekee. Ukiangazia barabara nchini utapata kuwa barabara nchini Kenya haziko katika hali nzuri . Zile za lami zimekuwa na mashimo makubwa ambapo mvua ikinyesha hufanya vidimbi mithili ya machimbo ya madini yaliyojaa maji baada ya kuachwa wazi. Na zile barabara zisizokuwa za lami zimeharibika kiasi kwamba ni vigumu kuzitofautisha na njia za ng'ombe kwenye maeneo kame.Kinachohitajika ni serikali kuzifanyia ukarabati ili kuzirudisha katika kiwango ambacho zitaweza kufaa tena.

Wananchi pia inafaa waelimishwe ili wasikubali kuingia kwenye magari ambayo tayari yamejaaa kupita kiasi. Hili litawasaidia wananchi wenyewe kudumisha usalama wao barabarani. Pia inafaa watambue ya kwamba wana jukumu la kuwaarifu walinda usalama endapo dereva anaendesha kwa kasi sana kuliko ile ya kilomita 80 kwa saa iliyokubaliwa.

Inafahamika kuwa maafisa wa uslama ndio wafisadi zaidi, hivyo basi huchangia katika kuongeza idadi ya vifo barabarani. Katika vita dhidi ya ufisadi na ajali za barabarani, ni mwananchi mwenyewe ambaye anawezesha kukomesha hali hii. Kwa mfano, afisa wa usalama akipatikana akichukua

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

hongo, yeye pamoja na yule aliyetoa hongo wapelekwe kwenye vituo vya kukabiliana na ufisadi na wachukuliwe hatua kali, matatizo haya yataisha.

Lakini kabla kufika hapo, ni muhimu kumhamasisha mwananchi kuhusu haki zake na namna ya kukabiliana na suala hili la ufisadi. Hali hii inatuonyesha kwamba mipango maalum inapaswa kufanywa na serikali ili kuwaelimisha wananchi kama hatua ya kwanza ya kukabiliana na ufisadi hatimaye izilainishe sekta zote wala si ya uchukuzi na mawasiliano pekee.

Maswali

(a) Mbali na ajali za barabarani, taja, tatizo lingine sugu ambalo linakumba nchi ya Kenya **(al.1)**

(b) Ajali za barabarani zinasababishwa na nini? **(al.4)**

(c) Mwandishi anapendekeza hatua zipi zichukuliwe na serikali ili suluhisho la kudumu lipatikane? **(al.2)**

(d) Taja hatua ambazo serikali imechukua ili kuimarisha uchukuzi **(al.3)**

(e) Ni kitu gani ambacho kinaonyesha kuwa serikali imeshindwa kukabiliana na ajali barabarani? **(al.2)**

(f) Eleza maana ya maneno haya:- **(al.3)**

(i) Tatizo sugu.
(ii) Vithibiti mwendo.
(iii) Machimbo.
(iv) Ukarabati.
(v) Hongo.
(vi) Kuhamasisha..

3 .Matumizi ya lugha (alama 40)

(a) Jaza mapengo:-

Kutenda	**Kutendesha**	
(i) Chota	.....	**(ala 1)**
(ii) Lewa	.....	**(ala 1)**

(b) Taja sauti moja ya; **(ala 1)**

(i) King'ong'o

(ii) Kiyeyusho **(al.1)**

(c) Tumia neno "*shujaa*" katika sentensi kama:- **(al. 1)**

(i) Kivumishi

(ii) Kielezi... **(al. 1)**

(d) Tambua vitenzi katika sentensi hii kwa kuvipigia mistari:- **(al. 2)**

Sisi tulikwisha kutambua alikuwa na nia mbaya. Yeye ndiye mwizi .

(e) Andika wingi wa sentensi hii katika hali ya ukubwa:- **(al. 2)**

Kichinjio hiki kilikarabatiwa kwa pesa nyingi

(f) Eleza maana mbili ya sentensi ifuatayo **(al.2)**

Wanafunzi waliwaaandikia barua

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

(g) Jaza neno ambalo ni kinyume cha lile lililopigwa mstari katika sentensi:- **(al.2)**

(i) Vile vitu **<u>ulivyovichanganya</u>** itakubidi …….

(ii) Bomba hili l**<u>imeziba</u>** mwite fundi aweze ……..

(h) Unganisha sentensi hii kwa kutumia *'O'* rejeshi :- **(al. 1)**

Wavu umekatika. Wavu ni wao

(i) *Eleza maana ya :-* **(al. 2)**

(i) Kiimbo:.

(ii) Shadda…

(j) Yakinisha sentensi hii: **(al. 2)**

Sijafahamu kwa nini hawamkaribishi mpwa wao.

(k) **Andika katika usemi halisi:-** **(al. 2)**

Mama aliwahimiza warudi siku hiyo la sivyo wangekosa tuzo

(l) Akifisha sentensi ifuatayo:- **(al.3)**

Sijaona kitabu kizuri kama mayai waziri wa maradhi, utaniazima siku ngapi bashiri alimwuliza rita

(m) Changanua kwa njia ya mishale. **(al. 4)**

Mama anapika na baba akisoma gazeti

(n) Panga nomino hizi katika ngeli mwafaka **(al. 2)**

(i) Kipofu.....

(ii) Uyoga.....

(o) Tambulisha kundi nomino na kundi tenzi ktika sentensi **(al.2)**

Wanafunzi watundu wanacheza darasani

(p) Pambanua viambishi mbalimbali katika sentensi ifuatayo **(al. 3)**

Waliwapendezea

(q) Eleza maana ya misemo:- **(ala. 2)**

(i) Fuga mtu –

(ii) Kuwa na faragha –

(r) Chai hiyo iliwavutia watalii (*Anza* : Watalii……..) **(al. 2)**

4)Isimu Jamii (al.10)

a) Lugha ya kiswahili inakabiliwa na matatizo mengi sana. Yataje na kuyaeleza.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

5) USHAIRI(ALAMA 15)

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata

1. Yawile matononofu majani, hali yoyote iwavyo
Yefura ukamilifu majani, yalikiota vilivyo
Pamoja yalimakifu majani, kwa jinsi mambo yendayo
Fahali kayatilifu majani, ndivyo igeuke sivyo
Wanapowana fahali ziumiazo n' nyasi

2. Ingawa yali dhaifu majani, pamoja yalishikana
Ama katika wakifu majani, au kwa kusaidiana
Ndugu yali bainifu majani, tokea zamani sana
Yakapondwa bila hofu majani, fahali walipowana
Wanapowana fahali ziumiazo n'nyasi

3. Pondaponda mepondeka majani, fahali wakivutana
Tena yakatawanyika majani, kwa jambo lisilo kina
Yakabaki kudhiika majani, ndugu wanaofanana
Fahali wanayacheka majani, wala habri hawana
Wanapowana fahali ziumiazo n'nyasi

4. Fahali wanapotaka yakini, hata hutembeleana
Na makoo kadhalika yakini, wanapotoka kuonana
Ndama pia watavuka yakini, ng'ombe ile kulishana
Tena nyasi hazochoka yakini, karibu kazikutana
Wanapowana fahali ziumiazo n' nyasi

5. Si ndaama si ukoka majani, si mbuga si wanda tena
Yamebaki mabaka majani, vipande kuoteana
Kwa machaka hazoshika majani, hayawezi kupachana
Na fahali watimka majani',ngali wakisuguana
Wanapowana fahali ziumiazo n'nyasi

Maswali

(a) Mwandishi ana ujumbe gani katika shairi hili? (al.1)
(b) Eleza muundo wa shairi hili. (al. 5)
(c) Mwandishi amefauluje katika kutumia uhuru wa kishairi? (al.3)
(d) Andika ubeti wa pili katika lugha ya nathari (al. 4)
(e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi (al. 2)
(i) Mabaka **(ii)**Kupachana

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM TWO HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 08

KISWAHILI
KIDATO CHA PILI
MJARABU WA KWANZA

1. UFAHAMU

Wahenga walisema “motto umleavyo ndivyo akuavyo”. Hii in maana ya kuwa ukiogopa kutumia ufito kumchapa motto wako, ukamdekeza, utadeka na hatimaye ataharibika. Methali hii ina pacha yake ambayo ni “ukicha mwana kulia, utalia wewe.

Hizi ni methali zilizojaa busara kubwa. Mathalani, wewe ni mzazi au mtu yeyote mzima aliyetunukiwa madaraka juu ya watoto, lakini kila wanapokiuka uadilifu au mmoja wao anapokosea wewe unambembeleza tu, basi huwa unaizorotesha tabia yake. Mtoto huyo anaweza kuishia kuwa mtundu.

Hata hivyo, ni sharti tujue ya kwamba tuko katika nji apanda hapa. Kwa upande mmoja, zamani ilichukuliwa kwamba watoto n ahata mzima ana jambo la kuwaeleza, njia pekee ya kuliingiza katika ‘akili yao’ ni kuwatwanga ili kulikongomeza jambo hili. Ukweli ni kwamba akili ya motto si hafifu hata. Unaweza kusema ni kam ammea, ambao usiporutubishwa kimakusudi, ukapaliliwa vyem ana kustawishwa stahiki yake, basi hudhoofu; na mwisho kufifia .

Kwa upande mwingine, mtazamo wa kisas ani tofauti kabisa. Imethibitishwa ya kiwamba wanawake ni sawa kabisa katika maumbile yao wakilinganishwa na wanaume. Kwa jinsi hiyo, kweli wapo wanawake ambao hawana mwelekeo timamu kuhusu maisha, lakini ni kweli kuwa watoto wote, kwa sababu ya umri wao tu, basihawana akili. Kadhalika, si kweli kuwa watoto wote, kwa sababu ya umri wao tu basi hawana akili. Ama kwa kusema kweli binadamu yeyote huzaliwa na akilipungufu. Hili litokeapo, basi tunalikubali tu. Hatuwezi kumlaumu mtu kama huyo au muumba wake. Kwa hakika huu ndio msingi wa methali, “akili ni nywele, kila mtu an azake.” Vinginevyo, mtazamo wa kizamani ni taasubi kongwe tu za kiume zilizopitwa na wakati.

Aidha, kwa sababu watu wote huzaliwa na akili timamu, tene hawawi watu wazima kabla ya kuwa watoto kwanza, mtu mzima yeyote an ahali gani ya kuwadhulumu watotro na kujipambaniza na lawama za uongo dhidi ya vijana hao kwa madai kuwa hawana akili? Na je, ikiwa hawana akili, basi ndipo waonewe? Wanyanyaswe? Hii si jambo la busara. Kurudi Mtoto kwa visa vya maonevu ni kumrudisha nyuma kiumbe huyo. Kurudi kufaako ni kwa kupeleka, sio kwa kurudisha nyuma. Kurudi kuelekezako mbele ni kwa uongozi ambao lengo lake ni kumulikia mtoto kurunzi ilimradi kumwangazia tariki njema.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Mtoto asinyimwe vya tunu vyovyote ambavyo ni stahiki yake, kwa kisingizio kuwa vimetengewa mtu mzima, ndugu mkubwa, mwalimu, au mtu awaye yeyote Yule aliyekabidhiwa jukumu la kumlea au mtu mzima, ndugu mkubwa, mwalimu au mtu awaye yeyeto. Yule aliyekabidhiwa jukumu la kumlea au kumwogoza motto.
Mtoto ana haki ya kuhudumiwa kwa njia yeyote ifaayo ili akue na akili yake ikomae kikamilifu. Inafaa asomeshwe,apewe malezi bora ili naye alee wengine kistahiki.

MASWALI

a) Mapenzi yasiyo kipimo yanaweza kuwa hatari kwa motto. Eleza kikamilifu huku ukirejelea habariuliyosoma . **(Alm3)**

b) Fafanua njia panda inayorejelewa na matunzi. **(Alm3)**

c) Mtoto analinganishwa na mmea katika taarifa hii, kwamba "usiporutubishwa kimakusundi, ukapaliliwa vyema na kustawishwa stahiki yake basi hudhoofu," tathmini kulinganishwa huku, huku ukirejelea taarifa. **(Alm3)**

d) Akili ni nywele, 'Kila mtu ana ;zake. Eleza maana ya ndani ya methali hii kulingana na taarifa. **(Alm2)**

e) Onyesha kwamba unaelewa maana ya: **(Alm2)**
Kurudi Mtoto kwa visa vya maonevu ni kumrudisha nyuma kiumbe huyo."

f) Eleza maana ya: **(Alm2)**

i) Kulikongomeza **ii)** Kujipambaniza

2. MATUMIZI YA LUGHA. (Alama 30)

a. Eleza tofauti ya kimatamshi baina ya sauti zifuatazo.

i) (K) ii) (G)

b. Eleza maana nne zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo. **(Alm4)**
Tande alimpigia milimo mpira

c. Sahihisha sentensi ifuatayo kwa njia tatu mwafaka. **(Alm3)**
Hapa Kwetu Mna Siafu Wengi.

d. Eleza maana ya ngeli. **(Alm1)**

e. Andika sentensi mbili ili kuonyesha maana tofauti za alama ya kibainishi. **(Alm2)**

f. Eleza maana ya mofimu. **(Alm2)**

g. Eleza hali zinazodhihirika katika sentensi zifuatazo.

i) Gari lake limebingirika mtaroni.

ii) Cha mlevi huliwa na mgema.

h. Andika sentensi ifuatayo kwa usemi taarifa. **(Alm2)**
"Hamjambo wanafunzi", mwalimu aliwasalimia

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

i. Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa. **(Alm2)**

Watoto walinunuliwa viatu maridadi.

j. Andika kinyume cha sentensi, **(Alm2)**

Shangazi alifurahishwa na wimbo huo.

k. Tunga sentensi kuonyesha maana ya vitale vifuatavyo. **(Alm2)**

i) Pamba

l. Toa maelezo ya msamiati ufuatao. **(Alm4)**

i) Kielezi

ii) Kiiunganishi

iii) Kiwakilishi

3. ISIMU JAMII

a) Eleza maana ya. **(Alm5)**

i) Sajili

ii) Lahaja

iii) Isimu

iv) Lafudhi

b) Eleza maana ya **(Alm5)**

Kuchanganya ndimi

4. FASIHI SIMULIZI (Alama 10)

a) Maigizo ni nini? **(Alm2)**

b) Toa mifano mine ya maigizo. **(Alm4)**

c) Taja Dhima nine za maigizo. **(Alm4)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM TWO HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 09

1. UFAHAMU (Alama10)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Tokea muundo mpya wa serikali ya ugatuzi uanze kutekelezwa miaka miwili iliyopita, kumeendelea kushuhudiwa matatizo mengi hali iliyopelekea kushuhudiwa kwamsururu wa migomo na maandamano ya raia. Fujo za karibuni kabisa ni zile zinazoshuhudiwa katika miji mikubwa za wachuuzi na wafanyibiashara wakipinga hatua za serikali za kaunti kuwatoza ushuru takribani kwa kila huduma na bidhaa ikiwemo wanyama, kuku na ndege. La kuhuzunisha zaidi katika baadhi ya majimbo imeripotiwa kuwa raia wamelazimishwa kulipa ushuru kwa kutaka tu kuona maiti za jamaa zao kwenye vyumba vya kuhifadhi maiti.

Wanasiasa wameonekana kuwa na wakati mgumu kutetea mfumo huu mpya wa ugatuzi huku baadhi wakisema kwamba matatizo yanayoshuhudiwa kwa sasa yametokana na ugeni wa mfumo huo. Wengine wameinyoshea kidole serikali ya kitaifa kwamba ndiyo inayosambaratisha muundo huu. Wengine wanahoji kuwa bado ni mapema na kwamba kunatajika muda mrefu ili kufaulu.

Ni wazi kwamba kumekosekana nidhamu bora ya kusimamia maisha ya raia nchini Kenya. Matatizo yanayokumba raia kwa sasa ni dalili kuwa mfumo wa serikali ya ugatuzi umeongezea chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu. Swali ni je, hadi lini nidhamu ya kusimamia raia itakuwa ni suala la majaribio na makosa?

Hatua ya kuwarundikizia raia ushuru mkubwa ni kitendo cha unyonyaji na cha dhuluma kinachofaa kupingwa. La kufahamishiwa hapa ni kwamba ushuru ndio njia kubwa ya kuzalisha mapato ya serikali zinazojifunga na mfumo wa kimagharibi wa kiuchumi wa kibepari ikiwemo Kenya. Asilimia 90 ya mapato ya serikali za kibepari huegemea ushuru. Kwa hivyo hatua ya serikali za kaunti katika kuwanyonya raia kwa kuwalipisha ushuru si ajabu bali ni thibitisho kuwa jamii ya Kenya inaongozwa na nidhamu ya kiuchumi ya ubepari mfumo wa unyonyaji na ukandamizaji. Ukweli unabakia kuwa ndani ya serikali za kibepari raia ndio hubebeshwa mzigo wa ushuru unaoishia matumboni mwa viongozi!

Miito ya mabadiliko ya katiba na ya miundo mipya ya kiutawala si lolote ila ni moja tu ya hatua za mfumo wa kibepari kujipa muda wakuishi na kuziba aibu zake za kushindwa kusimamia maisha ya watu. Kufeli huku kwa mfumo huu kunashuhudiwa hadi kwenye nchi kubwa za kibepari kama Marekani na Uingereza hivyo nazo zimekumbwa tele na maandamano na fujo za raia wakilalamikia hali ngumu ya maisha.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Maswali

a) Yape makala haya anwani mwafaka. **(alm1)**

b) Eleza mtazamo wa wanasiasa kuhusu utepetevu wa mfumo huu. **(alm 2)**

c) "Ugatuzi nchini Kenya ni mfumo wa kibepari" Thibitisha kauli hii kwa kurejelea makala. **(alm1)**

d) Migomo ni zao la matatizo yaliyogatuliwa kutoka kuu. Toa sababu nyingine zinazosababisha migomo katika serikali za ugatuzi **(alm 2)**

e) Thibitisha jinsi mfumo wa ugatuzi umeongeza chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu **(alm 2)**

f) Eleza maana ya neno lifuatalo **(alm 2)**

Ugatuzi

3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama30)

a) Tofautisha sauti zifuatazo. **(alm2)**

/a/ **/u/**

b) i) Ngeli ni nini? **(alm1)**

ii) Maneno haya yamo katika ngeli gani? **(alm2)**

(i) Tunda **(ii)** Kipepeo

c) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo **(alm3)**

Sikumkaribisha

d) Andika kwa wastani **(alm 2)**

Magoma hayo yatachezwa mawanjani

e) Tofautisha sentensi zifuatazo. **(alm2)**

i) Baniani mwenyewe ni huyu.

ii) Baniani mwenye mali amelejea.

f) Tunga sentensi ukitumia VIELEZI vya;na upigie mstari **(alm3)**

a) wakati **b)** mahali **c)** namna

g) Tunga sentensi kuonyesha maana mbili za neno

chuma **(alm2)**

4. **ISIMU JAMII (Alama 5)**

i) Eleza maana ya **Isimu Jamii** **(alm1)**

ii) Eleza sifa nne za mazungumzo kati ya daktari na mgonjwa. **(alm4)**

5. FASIHI SIMULIZI

(i) Eleza sifa sita za fasihi simulizi.

(ii) Ushairi ni kwa malenga.Taja watendaji wa tanzu hizi.

Nyimbo

Hadithi

(iii) Tofautisha kati ya:

Hurafa na Hekaya

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM TWO HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 10

1. **UFAHAMU** **(ALAMA 15)**

Soma taarifa ifuatayo halafu ujibu maswali

Kama kuna jambo ambalo limeiparaganya akili yamahuluki ni kuielewa dhana ya demokrasia. Kiumbe huyu heshi kuuliza mkururo wa maswali. Demokrasia ni nini hasa? Tunaweza kula demokrasia? Ni dude gani hili lina kichwa au mkia pekee yake? Je demokrasia inazuia njaa? Demokrasia ni himaya ya wasomi tu au vilevile ni haki ya mafalahi? Kwa muda mrefu kumekuwa na kinyang'anyiro kikubwa katika jamii ambacho azma na. matokeo yake yamekuwa ya kutatanisha. Baadhi ya watu wamejitokeza kama mchuzi wa ugali na kuzusha zahama ambazo si za kuyumkinika. Vichwa vya adinasi vikafyekwa kwa miundo na maparange na matumbo yakapasuliwa na kuapakaza utumbo na vijusi kila mahali. Shingo zikapigiwa vigingi na kukomewa ardhini. Demokrasia si mchezo wa lelemama. Ni sharti tujifunge vibwebwe tumwage damu na tufe ili tupate demokrasia ya kweli!" Mmoja wa mibabe wa demokrasia alinguruma kadamnasi ya umati huku ngoma za vita zikirindima." Hata Marekani na ulaya walimwaga damu. Mamilioni ya watu walipukutishwa na kimbunga cha demokrasia. Chini walilaliana kama Vimatu na tunutu. Hawa manafiki wanafikiri hatuwajui. Katu hatutakubali porojo zao. Wanatupikia majungu kisha wakatoweka. Kuna demokrasia ya Afrika na ile ya Ulaya ' mkereketwa wa Uafrika akachanganua.

Demokrasia ya Afrika basi imefuata mkondo huu wa umwagikaji damu. Kila kukijiri uchaguzi zahama hutawala. Walio madarakani hawataki kubanduka. Hutaruta visababu vya kukwepa wimbi la ushinde. Demokrasia ni mchezo wa mizengwe tu ati. Hali hil imesababisha maafa makubwa, uharibifu mkubwa wa mali, majeraha, ukimbizi wa raia ndani na nje ya mataifa husika, dhuluma za kimapenzi dhidi ya wanawake, kuzagaa kwa magonjwa ainati, uhasama wa kikabila. Jambo la kusikitisha ni kwamba raia na viongozi hawaelekei kujifundisha chochote kutokana na hali. Huku mataifa mengi Ulayani na Asia yakikwea daraja moja baada ya nyingine kimaendeleo, Afrika imedumaa tu. Imesalia kuimba ule wimbo wake wa kutokea azali' Tutaendelea vipi na tunadhulimiwa na kaka wakubwa". Siasa ya demokrasia katika bara la Afrika ina tija kubwa hususan kwa wale wachache wanaofanikiwa kudhibiti nyenzo za kutia tonge kinywani. Ulitima wa umma husalia miradi hewa ya tabaka la viongozi ambayo hutumiwa kujinadi zamu nyingine ifikapo tena. Demokrasia ya kweli imo mikononi mwa umma pale utakapojikomboa kimawazo na kwa ujasiri kudai huduma bora, uajibikaji na kuheshimiwa kwa mkataba wa kijamii uliosisiwa na Jean Jacques Rousseau.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Maswali

a) Binadamu amechanganyika kwa njia ipi) **(Alm2)**

b) Ni vipi Demokrasia ya kweli inaweza kufikiwa **(Alm2)**

c) Kwa nini inasemekana kuwa 'Demokrasia ni mchezo wa mizengwe? **(Alm2)**

d) Ni athari gani hutokana na kinyang'anyiro cha Demokrasia? **(Alm4)**

e) "Dhiki za raia zimesalia kuwa mradi-hewa wa wanasiasa" Eleza. **(Alm2)**

f) Fafanua maana ya maneno na mafungu yafuatayo jinsi yalivyotumika katika taarifa.**(Alm3)**

i) Mafahali

ii) Wanatupikia majungu

iii) Ukarabati

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali yanayofuata

Wakaazi wengi wa maeneo ya kitajiri miji yetu hawajui wapo chini ya utawala wa machifu.Huenda wakasalia katika hali hii ya kutojua hadi wanapokosa kulipa ujira wa watumishi wao wa nyumbani halafu maskini mwajiriwa huyu anaripoti kwa chifu, kwa kuwa ni hali yake. Chifu ni uzi muhimu katika vazi Ia kijamii. Bila hawa maafisa, jamii kama tunavyoijua ingeporomoka. Wakati mwingine hawaungwi mkono. Mfano mzuri ni kukataliwa kwa katiba kielelezo cha Wako, Novembe 2005, wakati wa kura ya maoni. Kwa sababu jukumu la chifu au kibadala chake halikudhihirishwa wazi wazi katika kielelezo, wengi walikataa stakabadhi hiyo, wakihofia sasa hawataweza kufikia mtawala wao kushughulikia malalamishi yao.

Nimeishi mtaa wa Nairobi West miaka mingi na kuhudhuria kamati nyingi za lokesheni, chini ya uwenye kiti wa chifu akisaidiwa na naibu na wazee. Mikutano, pia inahudhuriwa na madiwani, inspekta wa askari tawala na wawakilishi wengi na washia dau katika lokesheni. Takribani kila swali linalogusia maslahi ya jamii linajadiliwa na kuchunguzwa na maazimio kupitishwa. Mada muhimu wakati wa mikutano hii ni usalama, taa za barabarani, ulanguzi wa mihadarati hasa karibu na taasisi za elimu, kudumisha usafi wa vyoo vya umma, kudumisha usalama kupitia kwa raia na swala nyeti la vioski.

Kazi ngumu ya chifu ni kuwazia kila kju. Kwa mfano, mwenye kioski ni sharti apate mkate wa kila siku na sehemu ya biashara yake iliyoko ni muhimu. Ikiwa kioski kitajengwa na kukiuka sheria za baraza la jiji au ikiwa wizi usiofahamika na utumizi wa dawa za kulevya unatokea kufuatia kukua kwa idadi ya vioski katika eneo, shinikizo zinaelekezwa kukuwa kwa wenye vioski. Chifu lazima azingatie shinikizo za umma hatari za kiusalama na hofu za wenye vioski kabla ya kufanya uamuzi ikiwa mijengo hiyo ibomolewe.

Tatizo jingine ni watoto wa barabarani. Makao ya kuwakimu ni machache kama walivyo wahudumu wa kijamii, suluhu ni nini? Tuwatupe katika ukumbi wa kijamii, ambao watahepa pindi *tu*, wapatapo

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

fürsa ndogo au wapelekwe huduma kwa vijana wa Taifa, ambapo wachache wanaweza kutunzwa kwa wakati mmoja. Ili kufaulu kwa wengine, sharti wawe katika vituo vya urekebishaji tabia za matumizi ya dawa za kulevya. Tuwakabidhi polisi kwa sababu wanaranda au tujaribu kuungana na vituo vya urekebishaji tabia kuhakikisha hawatarudi barabarani.

Mazingira ya lokesheni pia huibuka katika ajenda. Hali ya barabara, juhudi za kusafisha mazingira, wizi wa maji na umeme, usafiri wa umma, uchafuzi wa mazingira, hewa na kelele, hii inatokea kupitia malalamishi ya watu wanaoishi karibu na mabaa na uzingativu wa saa ya biashara hujadiliwa kila mara. Chifu ni sharti afahamu sheria na kanuni zinazotawala hali hizo, halafu ajadili na wahusika kabla ya kutoa mwelekeo. Usawa na uwazi katika kugawa fedha za Hazina ya maendeleo ya maeneo Bunge, pia hujadiliwa.

Katika maswala haya mengine, chifu ndiye aliye nyanjani. Anawajibikia jamii na wakubwa wake na hatarajii shukrani au kutambuliwa kwa kazi njema aliyofanya. Isipokuwa hukashifiwa anapofeli. Watu wengine wana taswira ya Chifu kama mtu kwenye jukwa, kofia yake. na kifimbo kinachompa mamlaka ya kuhutubia baraza, Kajubu tyji zaidi ya hivyo. Kwa mujibu wa kitabu cha mafunzo ya machifu na Naibu wao (Januari 2004), wajibu wa chifu ni kuwakilisha sera na mipango ya serikali kwa wananchi. Chifu ni ajenti wa "mabadiliko" mwenye wajibu Wa kuhamasisha watu katika

maendeleo. Anajishughulisha na kujua ni nani maskini katika lokesheni, mkoa, mgonjwa asiyeweza kupata tiba na kupanga jinsi mhasiriwa atakavyopelekwa hospitali kama anavyoweza. Ni sharti ashughulikie ugomvi wa kinyumbani, uhalifu wa watoto, dhuluma za watoto, agawe chakula na mavazi kwa wahitaji na kuhukumu kesi ndogo za wizi na uharibifu. Chifu hutatua kesi za kisheria kwa wasioweza kumudu wakili. Wakati wananchi wanapohisi mbunge wao hafikiliki na hawana imani na polisi, chifu ndiye suluhisho.

Lakini kuna machifu wachache ambao hawafanyi kazi yao vyema. Kwa ufupi, chifu ni mkusanyiko wa kushngaza; mfalme katika himaya yake, pasta, baba msikivu, wanasaikolojia, mtunga sheria na mdumisha sheria, balozi mchaguzi, mama, mlumbi na askari asiyechelewa. Ingawa halipwi vyema, anafanya kazi bila tarakilishi, na aghalabu hujilipia gharama ya kodi ya afisi yake kutoka mfuko wake. Kwa sababu ni mtumishi wa *umma,* tunataraji afanye kazi mufti. Hiyo haimaanishi tusishukuru kwa kazi njema aliyofanya. Serikali inaweza kufanya hivi kwa kuimarisha hali yake ya kazi, mazingira yake ya kikazi, na kuhakikisha yana tarakilishi, anapata mafunzo ya uongozi na usimamizi. Wananchi sharti washukuru watu hawa kwa kujitolea sabili.

Maswali

a) Fupisha aya nne za kwanza (Maneno 60) **(Alama 6, mtiriko,1)**

b) Kwa maneno kati ya 80-90 fupisha aya ya tano hadi mwisho. **(Alama 9, mtiririko 1)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

3.MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a)i) Taja sauti mbili ambazo ni vikwamizo na hutamkiwa kwenye ufizi **(Alm1)**

ii) Taja sifa mbili bainifu za vokali 'U' **(Alm2)**

b) Yakinisha sentensi hii. **(Alm2)**

Simba asiponguruma wanyama wote hawababaiki.

c) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo uliyopewa. **(Alm2)**

Mbwa ambaye aliripotiwa kuwa ameibwa amepatikana katika bwawa la maji.

(Anza: Katika bwawa……..)

d) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mbinu ya matawi **(Alm4)**

Mwanafunzi stadi amenunua kitabu kizuri.

e) Ukizingatia neno lililo katika mabano, andika sentensi hizi katika hali ya kutendeka.

i) Daraja hili(vuka) tu wakati wa kiangazi **(Alm1)**

ii) Kitabu hicho(soma) ijapokuwa sura zingine hazimo. **(Alm1)**

f) Andika katika ukubwa wingi **(Alm2)**

Kitoto kijeuri kikiletwa kitarejeshwa kwao.

g) Andika katika usemi taarifa. **(Alm2)**

"Tutawatembelea wazazi wetu leo jioni" Leo alimwambia Asha.

h) Tunga sentensi ukitumia nomino zifuatazo pamoja na kivumishi ___ingine **(Alm2)**

i) dau

ii) urembo

i) Bainisha yambwa tendwa na yambwa tendewa katika sentensi hii. **(Alm2)**

Mbunge wa Mtondo Kaskazini atawajengea wanakijiji josho kisha aghurie mjini.

j) Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatavyo. **(Alm2)**

i) Nafasi viambata

ii) Visisitizi

k) Tumia neno dhahiri katika setensi kulingana na maagizo **(Alm3)**

Kama:

i) Kiambishi

ii) Kivumishi

l) Tunga sentensi ya neno moja yenye visehemu vifuatavyo vya sarufi. **(Alm3)**

i) Kiambishi kiwakilishi cha kiima

ii) Kiambishi kiwakilishi cha wakati uliopo

iii) Kiambishi kiwakilishi cha kitendewa/mtendewa

iv) Shina la kitenzi

v) Kiambishi cha kauli ya kutendesha

vi) Kiishio

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

m) Bainisha kirai nomino na kirai kivumishi katika sentensi hizi. **(Alm2)**

i) Nguo aliyonunua mzazi ni mpya.

ii) Kondoo mwenye manyoya mengi hupendeza.

n) Akifisha **(Alm3)**

sikukuu ya madaaraka nilikwenda eldama ravine kumwona yohana akasema atakuja kuniona pamoja na mkewe siku ya jumapili

o) Eleza tofauti za kimaana baina ya sentenzi hizi. **(Alm4)**

i) Jambazi kutoka dukani aliiba

ii) Kutoka dukani jambazi aliiba.

iii) Aliiba jambazi kutoka dukani.

(iv) Jambazi aliiba kutoka dukani.

p) Unda nomino mbilimbili kutokana na mizizi ifuatayo. **(Alm2)**

i) -f-

ii) -l-

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

a) Eleza maana ya lugha **(Alm1)**

b) Taja sifa nne za lugha **(Alm4)**

c) Eleza sifa za sajili ya maabadani **(Alm5)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

CALL AMOBI GROUP OF EXAMINERS @ 0743 333 000 OR 0706 851 439 TO ACQUIRE :









